

# Kwa nini kupata chanjo?

Kupata chanjo ni zana muhimu ya kupunguza hatari ya ugonjwa mbaya wa UVIKO-19.



## Nani anaweza kupata chanjo ya Uviko-19?

- ✓ Watu wenye umri wa miaka 5+ (12+ kwa dozi ya nyongeza)
- ✓ Watu ambao ni wajawazito na wanaonyonyesha
- ✓ Watu ambao kinga ya mwili ni dhaifu (*ongea na daktari wako ikiwa una maswali au wasiwasi*)

Chanjo imethibitishwa kuwa salama katika tafiti za kisayansi zilizohusisha maelfu ya watu, na katika ripoti kwenye dunia halisi. Ingawa watu wanaweza kupata madhara madogo ya muda mfupi (kama vile mkono kuuma, uchovu au maumivu), madhara makubwa ni nadra.

## Je, chanjo bado inafanya kazi?

Ndiyo, chanjo zinaendelea kufanya kazi yao. Ingawa bado inawezekana kupata UVIKO-19 baada ya chanjo, chanjo hiyo inapunguza hatari ya kuugua vibaya, kulazwa hospitalini na kifo, na husaidia kuzuia kuenea katika jamii zetu.

## Je, bado ninaweza kupata chanjo baada ya kupata UVIKO-19?

Ingawa maambukizi pekee yanaweza kutoa ulinzi fulani, chanjo baada ya kupona UVIKO-19 husaidia kuboresha mwitikio wa kinga ya mwili na inaweza kutoa ulinzi bora na wakudumu. Baada ya kuambukizwa, subiri siku 60 kwa dozi ya kwanza au ya pili, au siku 90 kwa dozi ya nyongeza.

## Kwa nini kupata dozi ya nyongeza?

- Pamoja na dozi mbili za chanjo, kinga dhidi ya kuugua sana hubakia kuwa juu lakini hii inaweza kupungua baada ya muda.
- Dozi za nyongeza zinaweza kuongeza mwitikio wa kinga mwilini na kutoa ulinzi bora dhidi ya maambukizi na magonjwa makali.
- Dozi za nyongeza husaidia kupunguza kuenea kwa virusi, ugonjwa mbaya, kulazwa hospitalini na kifo.

Kupata chanjo yako/nyongeza ni **bure**. Unaweza kuipata hata kama huna kadi ya afya.



## Ninawezaje kupata chanjo?

- Tembelea kliniki ya chanjo ya bila miadi ya Chama cha Famasia cha Nova Scotia: [pans.ns.ca/walk-covid-19-vaccine-clinics](https://pans.ns.ca/walk-covid-19-vaccine-clinics)
- Weka miadi ya chanjo mtandaoni: [novascotia.ca/coronavirus/book-your-vaccination-appointment](https://novascotia.ca/coronavirus/book-your-vaccination-appointment)
- Au piga simu 1-833-797-7772.  
**Huduma za ukalimani zinapatikana.**



## Unahitaji usafiri kwenda kwenye miadi yako ya chanjo?

Usafiri wa vijijini unaweza kusaidia kwa \$5 kwenda na kurudi. Tembelea [ruralrides.ca/find-a-ride](https://ruralrides.ca/find-a-ride).

Ilisishwa Aprili 19, 2022

Jifunze zaidi kwenye [nshealth.ca/coronavirusvaccine](https://nshealth.ca/coronavirusvaccine)

